# Athari ya Upokezi wa Matendo ya Utu kwa Binadamu: Mfano wa Riwaya za Said Ahmed Mohamed

**Peres Akello Obondo, Juliet Akinyi Jagero & Naomi Nzilani Musembi**
*Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Jaramogi Oginga Odinga, Kenya*

**Uwasilishaji wa Makala**
*Pokelewa: 2024-12-14*
*Rekebishwa: 2025-02-14*
*Kubalika: 2025-02-16*
*Chapishwa: 2025-02-17*

***Maneno Muhimu***
Athari
Binadamu
Utu
Viumbe wa kiuhalisiajabu

**Jinsi ya Kurejelea Makala:**
Obondo, P. A., Jagero, J. A. & Musembi, N. N. (2025). Athari ya Upokezi wa Matendo ya Utu kwa Binadamu: Mfano wa Riwaya za Said Ahmed Mohamed. *Journal of Kiswahili and Other African Languages*, *3*(1), 12-20.

*Copyright © 2025*
CC BY NC SA

**Ikisiri**
Ili pawepo na mahusiano mema kati ya binadamu, lazima pawepo na utu. Utu, hasa huhusishwa na binadamu. Hali kadhalika, huhusisha wema wowote unaomtendea mtu. Waandishi mbalimbali wa fasihi ya Kiswahili wamedhihirisha utu katika utunzi wao. Mtu anapopokea tendo la utu, huathirika kwa namna mbalimbali. Makala haya yanachunguza athari ya upokezi wa matendo ya utu kwa binadamu. Lengo kuu la makala ni kueleza binadamu anavyoathirika kwa njia mbalimbali kutokana na utu wa viumbe wa kiuhalisiajabu. Viumbe wa kiuhalisiajabu kama wanavyoitwa ni viumbe wenye sifa za kiajabuajabu. Ni viumbe tofauti na binadamu halisi na wenye nguvu fulani. Kutokana na nguvu hizo, huweza kufanya matendo mbalimbali. Makala iliongozwa na nadharia ya kiuhalisiajabu kama inavyofafanuliwa na Zamora na Wendy (1995). Muundo wa kimaelezo ulitumika huku eneo la utafiti likiwa fasihi ya Kiswahili, utanzu wa Riwaya. Sampuli ya kimakusudi ilitumika kuteua riwaya tatu za Said A. Mohamed hususan: *Babu Alipofufuka (2001), Dunia Yao (2006)* na *Nyuso za Mwanamke* (2010). Data ilikusanywa kutokana na kusoma riwaya hizo tatu zilizoteuliwa na kudondoa sehemu zilizolingana na malengo ya utafiti. Data ilidondolewa, ikanukuliwa, ikapangwa kisha kuchanganuliwa. Matokeo yalionyesha kuwa viumbe wa kiuhalisiajabu walidhihirisha utu kwa binadamu kwa namna mbalimbali na athari yake ikabainika. Utafiti huu unatoa mchango kwa walimu na wataalamu wa fasihi katika taaluma ya fasihi simulizi.

## Utangulizi

Utu ni hisia ya kujitunza pamoja na kutunza wenzako. Ni hisia zito zaidi kuliko upole na ukarimu. Ni uwezo wa kuweza kuhimili upungufu wa mwenzako kama yako (Hannush, 2021). Neno linalohusiana na utu ni Ubuntu. Neno Ubuntu linatokana na dhana "Umuntu" kutokana na lugha ya Kizulu ambayo inatafsiriwa kuwa "Mtu ni mtu kwa sababu ya wenzake." Dreyer (2015) anaeleza kuwa. Ubuntu ni sifa ya uzuri wa binadamu kwa binadamu mwenzake. Tangia awali, falsafa ya Ubuntu imekuwa ikiwaongoza Waafrika. Huonyesha jinsi binadamu hushirikiana na binadamu wengine, mazingira pamoja na Mungu muumba. Ni falsafa muhimu kwa binadamu kwa kuwa binadamu bila Utu huwa katili kwa viumbe wengine.

Utu ni dhana ambayo imetumika katika nyanja mbalimbali za kijamii: kisiasa, kijamii n ahata kiuchumi. Hutumika kukashifu matendo yanayokiuka haki za kibinadamu kama vile unyanyasaji. Vile vile hutumika katika sehemu zilizosheheni vita (Ujomu, 2024).

Waafrika wanaamini kuwa utu ni ujamaa na ushirikano . Vile vile ni suala muhimu ambalo linamtambulisha mtu kitamaduni na linapaswa kuelimishwa wanajamii wanapofunzwa kuhusu tamaduni zao (Olawumi et al., 2024).

Utu umepungua sana miongoni mwa binadamu. Sio tu katika mawanda ya afya bali katika mawanda yote anayohusishwa binadamu (Asch et al., 2021). Asch na wenzake wanaeleza kuwa wachache katika uwanda wa afya wanapinga kuwa utu ni jambo moja kuu linalohitajika katika uwanda huo. Kwa mujibu wao wanasisitiza kuwa kupokeza tendo la utu kwa wagonjwa huleta mabadiliko mengi katika hali yao ya afya. Hii ni kwasababu wagonjwa hao watameza dawa zao ipasavyo na kutii maelekezo wanayopewa na madaktari wenye utu.

Mtu anapopokea matendo ya utu kutoka kwa wenzake, huleta uwiano kati yao. Msila (2015), anataja kuwa Ubuntu ni dhana ambayo tu inaweza kushirikishwa kwa umati wa watu na wala si kwa mtu binafsi. Msila, anasema kuwa, athari ya Ubuntu itajitokeza wazi wapokezi wakiwa wengi kuliko mtu mmoja. Anaendelea kusema kuwa, tendo hilo hupokelewa kwa matendo mahususi yenye uzuri wa kimo ya yaliyotendeka. Msila anasisitiza kuwa, jambo hili litaweza kusaidia hata kurehemu watu kutokana na tabia mbovu.

**Mbinu za Ukusanyaji na Uwasilishaji wa Data**

Ili kupata matokeo ya utafiti huu, Data zilikusanywa maktabani kwa kudurusu na kuchanganuliwa kwa riwaya tatu za Said A. Mohamed, *Babu Alipofufuka (2001), Dunia Yao (2006)* na *Nyuso za Mwanamke (*2010). Usomaji wa kina ulifanywa kwa majarida na machapisho yalioandikwa kuhusiana na mada ya utafiti, malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia ya uhalisiajabu. Data iliyokusanywa ilinukuliwa, ikapangwa na kisha kuchanganuliwa ili kuafiki malengo ya utafiti. Mtafiti alichanganua athari ya utu wa viumbe hawa kwa binadamu katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001), *Dunia Yao* (2006) na *Nyuso za Mwanamke* (2010) katika mkabala wa nadharia ya Uhalisiajabu. Data iliyokusanywa iliwasilishwa kwa njia ya maelezo na maandishi.

**Msingi wa Nadharia**

Makala haya yanaongozwa na nadharia ya Uhalisiajabu. Zamora na Wendy (1995) wanatueleza kwamba nadharia hii iliasisiwa mwaka wa 1925 na Mjerumani aliyejulikana kama Franz Roh aliyekuwa mhakiki wa sanaa. Franz Roh alitumia istilahi uhalisiajabu katika muktadha wa sanaa kuelezea na kuonyesha jinsi ya kusawiri aina fulani ya uujiza uliomo kwenye uhalisi uliozoelewa na unaotokana na ujarabati.

Kwa mujibu wa Zamora na Wendy (1995) nadharia hii ambayo pia hujulikana kama nadharia ya uhalisia mazingaombwe ni mojawapo ya nadharia za Usasaleo. Nadharia za Usasaleo hushikilia kwamba kazi ya fasihi hujengwa kutokana na kuchanganya mambo ya kiuhalisia na mambo yasiyo ya kiuhalisia. Nadharia hii ina mihimili yake ambayo imetokana na kazi za Danow (1995), Cooper (1998) na Zamora na Wendy (1995). Hivyo, utafiti huu uliongozwa na mihimili ifuatayo:

Mhimili wa kwanza: Katika nadharia ya uhalisiajabu, ndoto huchukua nafasi muhimu sana kwani matukio mengi hutokea wakati mtu anapolala au yumo mawazoni. Uhalisi na ndoto vinachanganyika. Khan (2023) anaeleza kuwa, ndoto ni mtiririko wa mawazo ya ndani ya mtu aliye macho au anayelala yanayoambatana na maono, taswira za matukio, mazingaombwe, fikira za uwongo, udhanifu, ndoto za mchana, ukisiaji, uwepo na malengo, matarajio na matamanio.

Mhimili wa pili: Matukio hayafuatani kimantiki kama ilivyo kawaida. Jambo hili hufanywa kwa kutumia mbinu ya ukumbukaji, mbinu rejeshi, mtiririko wa urazini na ujenzi wa wahusika wenye nafsi mbili. Mwandishi hutumia mbinu rejeshi kuvunja mtiririko wa vitushi (Punpeng, 2024).

Mhimili wa tatu: Simulizi zote hutegemea uhalisia ambapo kazi za fasihi za uhalisiajabu husimulia mambo ya kiajabuajabu na ya kutisha kwa namna ya uhalisia na ukawaida. Hivi, katika matini ya uhalisiajabu, jambo lolote huweza kujiri wakati wowote. Matokeo haya ya kiajabuajabu huonekana kuwa ya kawaida, pia huwa na hali za kushangaza, kuduwaza na kuogofya (Juwairina & Ekalestari, 2024).

Mhimili wa nne: Fantasia au uhalisiajabu hutumia taswira kujengea msomaji picha mawazoni mwake na kumwezesha kutafakari kuhusu matukio hayo yanayotokea (Rajabi et al., 2020). Mihimili iliyoelezwa hapa inawasilisha mawazo katika nadharia ya uhalisiajabu yaliyoongoza uchunguzi wa athari ya utu wa viumbe wa kiuhalisiajabu kwa binadamu katika riwaya teule za Said A. Mohamed.

**Matokeo ya Utafiti**

Kazi ya fasihi ya Uhalisiajabu husimulia mambo ya kiajabuajabu na ya kutisha kwa namna ya uhalisia na ukawaida. Matokeo haya huweza kushangaza, kuduwaza na kuogofya. Viumbe wa kiuhalisiajabu wamedhihirishwa wakionyesha utu. Utu wa viumbe hao umedhihirika kuwa na athari kwa binadamu. Aidha, binadamu akiwa amepokea tendo fulani huathirika kwa njia tofauti. Athari huweza kuwa chanya ama hasi. Hii hujitokeza kulingana na tendo alilopokea mtu. Sehemu hii basi imeshughulikia athari ya utu wa viumbe wa kiuhalisiajabukwa binadamu katika riwaya teule za Said A. Mohamed na zimejadiliwa ifuatavyo:

***Ushirikiano***

Ushirikiano hudhihirika baina ya watu wanaoelewana kuhusu jambo fulani. Ushirikiano ni sifa mojawapo muhimu katika maisha ya binadamu. Ni vizuri kuwa na ushirikiano kati yako na watu walio kwenye mazingira yako.

Marafiki wa dhati hushirikiana kwa njia mbalimbali. Katika riwaya ya *Dunia Yao* (2006), Ndi- anaeleza kuwa alichelewa sana kufika nyumbani baada ya kupata hela alizopewa na Shaib. Hela hizi alizipata kwa njia ya kiajabuajabu. Anaeleza kuwa alijikuta akipiga kipochi chake teke na alipokiokota akaona shilingi hamsini na tano, na huo ukawa muujiza kwake. Alipojiuliza alizipataje hela zile, Shaib alimjia kichwani na kumwambia kwamba pesa hizo alimsaidia baada ya kumwona Ndi- amekwama. Hili linathibitishwa na maelezo kutoka kwa Zamora & Wendy, (1995) ambao wanaeleza kuwa simulizi zote hutegemea uhalisia ambapo kazi za fasihi za uhalisiajabu husimulia mambo ya kiajabuajabu na ya kutisha kwa namna ya uhalisia na ukawaida.

> Leo nilichelewa kurudi. Si kwa kukimbia jukumu langu, lakini zaidi kwa sababu ujanadume wangu wote uliishia shilingi hamsini na tano mfukoni nilizogawiwa na Shaib, majununi mwenzangu. Nilijikuta tu nakipiga teke kipochi na nilipokiokota nikaona shilingi hamsini na tano. Huu ulikuwa muujiza kwangu, na nilipokuwa nikijiuliza ilikuwaje mtu kuangusha kipochi cha pesa katika dunia hii, Shaib alinijia kichwani na kung'ang'ania kwamba pesa hizo alizidondosha yeye, baada ya kuona nimekwama! (Uk 19).

Ndi- na Shaib ni marafiki ambao wanapendana, wanasikilizana, na wanasaidiana. Wanapatana kwa vyovyote vile na kila mmoja anamwelewa mwenzake. Licha ya Shaib kumsaidia na pesa, wanaonekana barazani wakiketi na Shaib, wakisimuliana hadithi. Mazungumzo yao hapa barazani yanamsaidia katika kupanua mawazo ya uandishi. Utu humsukuma mtu kumsaidia mwenzake mwenye maumivu ya kimwili, kifikra na hata ya kiakili. Kwa mujibu wa Obondo et al. (2022) utu ni sifa muhimu katika mahusiano ya binadamu, uhusisha wema na tabia njema. Vile vile, utu una sifa za upole, unyenyekevu, maarifa na uvumilivu. Shaib anaonekana na sifa hizi na anamsaidia Ndi-Kifedha na kimawazo.

K, katika riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001), anapopelekwa kwa dunia ya mzuka iliyo tofauti na dunia yake, anaanza kuelewa anachoambiwa na mzuka. Hii ni baada ya mzuka kumfafanulia jinsi wanavyoepukana na binadamu wenzao kwa kuwa wao ni tajiri na wengine ni maskini. Mzuka anamweleza utengano uliopo baina ya matajiri na maskini. Anamwelezea kuwa hiyo ni hatari wanayojilimbikizia. Anajaribu kumweleza kuwa si vizuri kutengana na binadamu mwenzako kwa sababu ya mali.

> Nani basi atakuja kumwambia kwamba zamani hakukuwa na kudhulumiana? Kwa upande mwengine lakini ilimjia wazi picha ya usamehevu iliyokuweko wakati ule ambayo leo katika wakati wao anajua wazi haipo. Na kwa msingi huu, babu yake mzuka alikuwa akisema kweli (Uk 101).

K alipuuza sana kauli hiyo. Ghafla lakini, kama kupwesa, jambo la ajabu lilimzukia. Macho yake haraka yalikuja kuripuka mripuko mkali; kama ule unaometa katika kiini cha juakali. Ndani ya kichwa chake mkafuatia mripuko wa radi iliyofuatia huo mweso. Alipeleka vidole vyake machoni akayafikicha, na alipoviondoa vidole, alianza kuhisi anafahamu yote aliyokuwa akiambiwa na mzuka sasa. Taswira ya anavyojifanya K kabla ya mzuka kupasha habari yake inajitokeza. Katika kazi za fasihi, fantasia au uhalisiajabu hutumia taswira kujengea msomaji picha mawazoni mwake na kumwezesha kutafakari kuhusu matukio hayo yanayotokea (Rajabi et al., 2020).

Baada ya hayo, K anaonekana kukubaliana na mzuka kuwa asemayo ni kweli. Si kwamba hakuyafahamu tokea mwanzo, lakini sasa alihisi hana hiyari kukiri ukweli wa mambo. Yaani hakuwa na kizuizi ndani ya nafsi yake. Kama vile kulikuja fagio lililosafisha ukaidi wake ndani kwa ndani. Kule kuona kwamba kila alichokuwa akisema na kukifanya mzuka sasa kilikuwa sahihi. Pamoja na hayo hakutaka kujionyesha kwamba anamfahamu. K anakubali kushirikiana na mzuka, vile vile anakubaliana na wazo la Mzuka kuwa matajiri wanadhulumu wasiojiweza.

***Furaha***

Kufurahia ni hali ya uchangamfu, kuridhika au kustarehe. Mtu haswa hufurahia tu jambo zuri linapotokea. Mtu huweza kufurahia kwa sababu ya mambo mengi.

Katika riwaya ya *Dunia Yao* (2006), Ndi- amefurahia sana usaidizi wa Bi Muse, baada ya kumtembeza katika bustani ya kimazingaombwe na kumwelimisha kuhusu masuala ibuka yanayohusiana na utunzi upya wa kisanaa wa kimazingaombwe. Ndi anaeleza kuwa:

> Naam, nilikiri. Hii ndiyo itakuwa simulizi yangu mpya katika mchanganyondimi. Kipande hapa…kipande pale. Vipande vya 'allegory'. Vipandevipande vya ngano mpya. Ngano ya tafrani- za kileo katika usogori mpya. Aaaaa, ikiwa zamani sikukujua Bi Muse, sasa nakuhitaji mara milioni moja. Nataka niwe nawe pachapacha. Nikukumbatie unikumbatie, unikoleze ilhamu, nilimwambia. Nikamsikia akicheka (Uk 68).

Kutokana na dondoo, Ndi- ana furaha tele. Furaha hii imetokana na usaidizi alioupata kutoka kwa Bi Muse. Ameona umuhimu wa Bi Muse kwake. Anasema kuwa sasa anamhitaji mara nyingi, awe karibu naye ndiposa aweze kuendelea kumsaidia katika uandishi wake. Katika wanda la uandishi na elimu kwa jumla, mtu huhitaji usaidizi wa wenzake ili kukwea kufikia kiwango alichofikia. Watu wenye tajriba aghalabu huwasaidia wale wanaochipuka katika mawanda mbalimbali.

Vile vile, Nana anafurahia kuvunja ungo. Hii ni katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (2010). Alikuwa msichana wa miaka ishirini na moja ilhali hakuwa amevunja ungo. Hakuwa ameingia miezini. Yanayomtendekea Nana hadi anavunja ungo ni mambo ya kiajabu ambayo yamehusishwa katika

masimulizi ya kiuhalisia. Kwa mujibu wa Punpeng (2024). Matukio ya kiajabuajabu huwasilishwa kana kwamba ni ya kawaida. Anafurahia kwa kusema:

> Nimeingia miezini… Nimeingia miezini! Baada ya miaka ishirini na moja nimezaliwa upya! ... Nimezaliwa upya! ... Nimezaliwa upya… Sasa nimeshakuwa mwanamke kamili… Nimeshakuwa mtu mzima! (Uk 29).

Nana alikuwa anajihisi mpweke. Alikuwa hana furaha kwa kuwa hakuwa amevunja ungo kama wasichana wenzake pale shuleni. Alikuwa chumbani pake na akimfikiria mamake akilini mwake. Hakutaka kumsikia mamake wa kambo na babake. Akiwa chumbani anahisi tu kuongozwa kwa lile apaswalo kufanya. Anafanya kila kitu anavyoelekezwa. Anapomaliza kufanya anavyoelekezwa na marehemu mamake anavunja ungo na anaingia mwezini. Anafurahia na kuanza kusherehekea. Kuingia kwake mwezini kulitokana na usaidizi wa marehemu mamake, suala ambalo linamfanya afurahie kupindukia. Mambo haya ni ya kiajabu kwa kuwa mwanamke huingia mwezini anapovunja ungo bila nguvu zozote kuhitajika.

***Shukurani***

Binadamu hushukuru anaporidhika baada ya kutendewa tendo fulani. Mara nyingi hushukuru tu anaporidhika na tendo jema analotendewa. Shukrani ni kitu muhimu sana katika maisha ya binadamu. Ni ishara nzuri kwa anayekutendea jambo. Humfanya mtu kuwa na ari ya kukusaidia tena kwa wakati mwingine. Watu hushukuru kwa njia mbalimbali. Huweza kushukuru kwa neno tu kama "Asante" au "Shukrani". Wakati mwingine huweza kushukuru kwa kukupa kitu fulani au kwa kukutendea jambo fulani kuonyesha ishara ya shukurani.

Nana anashukuru katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke (*2010), baada ya ishara anazopewa na marehemu mamake kumsaidia. Nana anasema hivi:

> Baadhi ya siku unapotaka kunikumbusha kitu, wewe huangusha kifaa chochote kwa kishindo: kikombe, kisahani, bilauri, bakuli, kitabu, kichupa, kioo, hata saa ya mezani. Nami hutambua ni wewe unayenikumbusha. Mara nyingine wewe huja ghafla kuniguta kwa jambo la hatari ninalolikabili- nami hukushukuru (Uk 18).

Taswira halisi inadhihirika wakati ambapo marehemu mama hutaka kujitokeza kwa Nana. Matukio haya yanapotendeka, yanaashiria ujio wake marehemu mama. Matumiza ya taswira ni miongoni mwa ufundi wa maandishi wanayotumia watunzi wa kiuhalisiajabu. Mara nyingi, marehemu mamake hujitokeza kwake Nana kumkumbusha kuwa anapaswa kufanya kitu fulani na hata humuonya kwa jambo la hatari linalomkabili. Baada ya usaidizi, Nana hushukuru.

Kutoa shukrani ni jambo muhimu sana maishani mwetu. Ikiwa utapata usaidizi wowote kutoka popote, ni vyema umshukuru aliyekusaidia. Hivi atakuwa na azma ya kukusaidia wakati mwingine tena ukihitaji msaada.

***Nguvu***

Huku ni kuwa na uwezo wa kufanya jambo au msukumo mkali unaotokana na nishati (TUKI, 2013). Binadamu wakati mwingine hufa moyo kutokana na mambo fulani. Jambo zuri nalo ni kuwa, wakati mwingine hupata nguvu au msukumo wa maisha kutokana na hali fulani. Kwa mfano, utamaushi katika maisha ya wanandoa huwa nadra. Hii ni kwa sababu, watoto ambao huwa zao la ndoa huwapa nguvu.

Dreyer (2015), anaeleza kuwa: Waafrika wanaamini kuna nguvu za ajabu ambazo hutoka kwa kiumbe wa ajabu mwenye nguvu na uwezo zaidi. Kiumbe huyu tena husambaza nguvu zake kwa viumbe

wengine au kwa vifaa. Kwa mujibu wa Juwairina & Ekalestari (2024), kazi za fasihi za uhalisiajabu husimulia mambo ya kiajabuajabu na ya kutisha kwa namna ya uhalisia na ukawaida.

Mwandishi wa a riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (2010), basi anadhihirisha hili kupitia Nana ambaye baada ya mamake kumzuru alipokuwa mchovu wa maisha na jamaa zake wakadhani kaelekea kufa, alipata nguvu tena baada ya masimulizi ya mamake kwake. Mamake alimzuru kumwonya kuhusu ndoa na akamzuru tena kumshukuru kwa jitihada zake kama mwanamke. Mwandishi anaeleza kuwa:

> Simulizi ya Bi Mkubwa ilipofika hapo, Nana alijiona anapasua ule ungozi uliokuwa ukimzuia kuingia chumbani mwake. Alipotazama vizuri aliona yuko juu ya kitanda chake, amezungukwa na kila mtu aliyeshtahiki kumzunguka: Amour, Faisal, Bi Chuma, bibiake, Bi Mau mama wa bibiake Bi Chuma na wenzi wengine waliokuwa wakiishi humo.Wote walikuwa wamechanua furaha kwa vile amemudu kuja juu kutoka chini kwenye sakafu ya dunia (Uk 292).

Nana amejigaragara sakafuni na kila mtu akawa na hofu pale nyumbani. Baada ya marehemu mamake kumzuru, ananyanyuka kutoka pale chini kwenye sakafu. Kila mtu pale nyumbani anafurahia. Nana amepata nguvu tena. Suala hili linajitokeza kama tukio la kawaida. Kuamka kutoka kwa maumivu fulani kwa kumwona mzuka tu si jambo la kawaida maishani mwa binadamu.

Katika riwaya ya *Dunia Yao* (2006), kuwepo kwa Bi Muse karibu na Ndi- unampa jazba ya uandishi. Ndi- anajisemesha, anasema:

> … Je, huu mkabala wangu na Bi Muse ni muhimu? Nani Bi Muse? Kiumbe gani huyu hasa? Ndiyo, jina lake nimekuwa nikilisikia na kulisoma siku nyingi. Kama alivyosema mwenyewe, si kiumbe wa sasambura turore. Hujifichua anapohitajiwa kwa mapenzi ya dhati au kwa kutoa msaada. Na mimi, nimefika baleghe ya kusalitika naye. Nina haja naye. Ninamhitaji. Ninataka anisaidie. Anisaidie kuwasaidia wengine ikiwezekana. Anisaidie kuukata ugumba wa utunzi. Nina hamu kurutubisha na kutia mbolea pahala fulani. Nipate kizazi kipya cha sanaa katika ukame wa ubunifu. Nipate kurutubisha kizazi kipya cha utu katika ukame usio na utu. Ninahitaji mtekenyo wake unipe jazba (Uk 62).

Ndi- anahitaji jazba katika utunzi wake. Ndi anataka kujua kutunga kazi zake kwa mfumo mpya na kwa ubunifu wa hali ya juu, na ni Bi Muse tu ndiye anayeweza kumsaidia. Ndi anahitaji mtekenyo wa Bi Muse umpe jazba ya uandishi. Anataka Bi Muse awepo ampe moyo wa uandishi wa kizazi kipya. Bi Muse ambaye ni kiumbe wa kiajabuajabu alikuja kwake kumsaidia katika sanaa yake ya uandishi. Kupitia kwake Bi Muse anaweza kutenda mengi katika sanaa ya uandishi. Ndi basi amepata nguvu mpya katika uandishi wake.

***Kushangaa***

Mtu anaposhangaa huonyesha hisia kutokana na kitu fulani. Kushangaa ni hali ya kuduwaa na kutojua la kufanya kutokana na jambo lililotokea. Watu hushangaa kwa njia tofauti, huweza kumaka kwa sauti au hata kutumia tu ishara za uso. Pia hushangazwa kutokana na matendo fulani yanayomtendekea. Matendo ya utu wanayopata wahusika mbalimbali yanawaacha kinywa wazi.

Katika riwaya ya *Dunia Yao* (2006), Ndi- anashangazwa sana na Bori. Anashangazwa na uwezo wa Bori kuzungumza namna ile. Bori ni mtoto wa Ndi-. Katika hali ile anapozungumza, amenyanyuka kutoka kwenye albamu. Kunyanyuka kwake kutoka kwenye albamu na kuzungumza namna ile si suala la kawaida. Babake, Ndi- vile vile anakuwa na mshtuko. Watoto wa Ndi- pamoja na mkeo

wanaonekana wakitoka kwenye albamu na kufanya shughuli za binadamu wa kawaida. Utu unajitokeza kupitia kwake Bori. Maneno yake yanamsaidia Ndi- kukuza falsafa yake ya uandishi.

> Niliemezwa kwamba Bori aliweza kusema namna hii. Ilikuwa kama miaka yote hii akienda macho wazi kuduhushi kila alama ya falsafa ya elimu na kuifundika kwenye bindo la unyamavu wake. Na sasa bindo hilo limejaa na kufufurika (Uk 114).

Anashangaa kwa kuwa Bori alichukuliwa tu kama mtoto ambaye alipenda kufanya vitu vya mkono kuliko kuongea. Kila wakati alipatikana akiwa ameketi akitengeneza vifaa kwa vyombo vya kuokotwa. Alisikika akiongea kwa nadra.

Uandishi wa kiuhalisiajabu mara nyingi haufuati mfuatano wa matukio kimantiki. Mwandishi hutumia mbinu rejeshi kuvunja mtiririko wa vitushi (Punpeng, 2024). Katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (2010), Marehemu mamake Nana, anamhadithia kuhusu maisha yake alipokuwa hai. Anamsimulia mambo yakusitisha aliyopitia katika ndoa na kumkanya dhidi ya kuingia katika ndoa. Utu wa mamake mzazi unadhihirika wazi anapojitokeza kumkanya kutokana na kuolewa. Linalomshangaza Nana ni uhusiano uliokuwepo kati ya mamake na babake. Anamwelezea ya kuwa:

> Licha kuolewa na Bwana Hila kwa nguvu za utajiri na mali yake, bwana huyo alidhani tu maisha ya mwanamke ni kustareheshwa. Kwa hali hii aliudhika. Alinigeuza mtawa nyumbani kwa kufanyiwa kila kitu na watumishi. Nilichukua vigae na kusaga na kumtilia kwenye chakula. Babako basi akanifukuza. (Uk 289)

Aliendelea kuishi maisha ya mateso hadi akawa na kiwewe. Alichukuliwa na kupelekwa kwenye hospitali ya wendawazimu kwa miaka. Hatari yake ilipopungua, alitolewa kwenda kuishi maisha ya kawaida. Nana anashangazwa kuwa babake ndiye aliyekuwa sababu ya mamake kuwa mwendawazimu. Anashangaa kwa kugundua kuwa kumbe Faisal ndiye aliyempenda mamake kwa dhati.

Kushangazwa kwa Nana kumetokana na maelezo ya mamake kuhusu ndoa. Marehemu mamake Nana anampenda mwanawe na hivyo kumtahadharisha kuhusu maisha mbaya ya ndoa. Hamtakii mabaya kama alivyopitia. Suala hili la kumtahadharisha linaonyesha utu alio nao.

***Kutoelewana***

Huku ni kutopatana kimawazo baina ya watu wawili, vikundi viwili au zaidi. Binadamu huwa na mawazo tofauti tofauti kuhusu dhana mbalimbali. Wakati mwingine, hukubaliana kuhusu mawazo haya na wakati mwingine huwa hawakubaliani na mawazo haya. Iwapo hakuna kukubaliana kuhusu jambo fulani, basi huleta kutoelewana kati ya watu.

Katika riwaya ya *Nyuso za Mwanamke* (2010), Nana anakataa kuamini wasemavyo watu kuwa mamake ni mfu. Anahisi yu hai kwa sababu amekuwa akipokea matendo ya utu kutoka kwake. Jambo hili linaleta kutoelewana kati ya Nana na watu wengine. Kutokea kwa mfu kwa binadamu aliye hai si jambo la kawaida ingawa yanatukia kwa wingi katika riwaya hii. Marehemu mamake Nana anajitokeza kwa Nana kila wakati. Vile vile, taswira inajitokeza ya matukio yalivyo muda mchache kabla ya ujio wa marehemu mamake Nana.

> Mara nyingi hukumbuka pale unapofurutu ada. Pale unapokuja kuninyukua au kunizaba kibao ili kunizindua na hatari inayonikabili. Nami hujua ni wewe kwani hapana mwingine ambaye angethubutu kunikamata mkono kunivusha barabara ya hatari. Na ingawa hulalama na kulaani huku nasugua mchonoto pajani au shavuni, hujikuta hatimaye nimeonyeka. Nimenusurika. Nimeepuka hatari. Kwa nini basi niwasikilize wao? Kwa nini niamini kuwa

> wewe haupo? Kwa nini nikubali umeshatoweka? Kwa nini nifanye hivyo wakati najua upo nami' karibu au mbali? (Uk 19).

Nana anakataa kuamini kuwa mamake hayupo. Hii ni kwa sababu kila wakati anahisi kuwa yupo karibu naye kutokana na zile ishara. Nana anashuku kuwa mamake yu hai na wala sio mfu. Hii ni kwa sababu kila anapohitaji msaada hupata na ni marehemu mamake ndiye humpa msaada.

**Hitimisho**

Utafitu huu umeweza kubaini athari zilizojitokeza kutokana na utu wa viumbe wa kiuhalisiajabu kwa binadamu. Imebainika kwamba matokeo haya ya utu hupokelewa kwa njia tofauti tofauti, chanya au pia hasi, ila wakati mwingi, utu hudhihirisha matokeo chanya. Kutokana na tendo hilo la utu, walioonyesha utu kwa wenzao walipata matokeo chanya kama vile: utiifu wa maelekezo waliotoa. Baadhi waliotii walipoonywa waliweza kusaidika. Wahusika wengine waliweza kutoa shukrani kwa wale viumbe, kwa sababu ya kuwaonyesha utu. Wahusika wengine waliweza kufaulu na kuishi maisha mema maishani kutokana na msaada waliopata kutoka kwa viumbe hawa. Mkondo wao wa maisha uliweza kubadilika baada ya wao kufuata kila agizo walilopewa na viumbe wa kiuhalisiajabu. Pia waliweza kuepuka hatari zozote zilizowakabili baada ya kuonywa na viumbe hawa. Kuna waliopokea tendo la utu na ikawaathiri kwa njia hasi pia. Mzozo wakati mwingine ulijitokeza kati ya kiumbe na binadamu aliyekuwa akipokea tendo la utu. Wakati mwingine, alipolemewa binadamu, alimalizia tu kwa kukimya kama aliyekuwa hasikilizi chochote.

**Marejeleo**

Asch, S. M., Atkins, D. V., & Walling, A. (2021). If Kindness Were a Drug, the FDA Would Approve It. *Journal of General Internal Medicine*, *36*(2), 263–264. https://doi.org/10.1007/S11606-020-06343-7

Cooper, B. (1998). *Magical Realism in West African Fiction.* Routledge.

Danow, K. (1995). *The Spirit of the Carnival; Magical Realism and the Grotesque.* Kentucky University of Kentucky Press.

Dreyer, J. (2015). Ubuntu: A practical theological perspective. *International Journal of Practical Theology*, *19*(1), 189-209. https://doi.org/10.1515/ijpt-2015-0022

Hannush, M. J. (2021). Kindness: *The Capacity for Kindness* (pp. 167–187). Palgrave Macmillan, Cham. https://doi.org/10.1007/978-3-030-74315-4_10

Juwairina, S. I., & Ekalestari, S. (2024). Magical realism elements in Dianna wynne jones' novel howl's moving castle. *Journal of Language.* https://doi.org/10.30743/jol.v6i2.10018

Khan, R. H. (2023). *Magical Realism in Indian Literature*. https://doi.org/10.52783/tjjpt.v44.i3.625

Mohamed, S. A. (2001). *Babu Alipofufuka.* Jomo Kenyatta Foundation.

Mohamed S. A. (2006). *Dunia Yao*. Oxford University Press.

Mohamed, S. A. (2010). *Nyuso za Mwanamke.* Oxford University Press.

Msila, B. (2015) Ubuntu and its potential impact on the international social work profession. International Social Work. 64 (5), 649-662. Doi: 10.1177/00208728211022787.

Obondo, P., Jagero, J. A., & Musembi, N. N. (2022). Utu wa Wahusika Viumbe wa Kiuhalisiajabu: Mtazamo wa Mwandishi Said Ahmed Mohamed. *East African Journal of Swahili Studies*, *5*(2), 131–141. https://doi.org/10.37284/jammk.5.2.1014

Olawumi, K. B., Mavuso, M. P., & Duku, N. S. (2024). Situating Ubuntu Philosophy in Pre-service Teacher Education. *International Journal of Learning, Teaching and Educational Research, 23*(8), 605–623. https://doi.org/10.26803/ijlter.23.8.31

Punpeng, G. (2024). Staging anxiety through magical realism: *A practice-based exploration in two theatrical productions*. https://doi.org/10.69598/hasss.24.3.270801

Rajabi, A., Azizi, M., & Akbari, M. (2020). Magical Realism: *The Magic of Realism.Rupkatha Journal on Interdisciplinary Studies in Humanities, 12*(2). https://doi.org/10.21659/RUPKATHA.V12N2.18

TUKI. (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Oxford University Press.

Ujomu, P. O. (2024). 'Ubuntu' African Philosophy or 'Ubuntu' as a Philosophy for Africa. *Journal Philosophical Alternatives,* XXXIII (5). https://doi.org/10.58945/uyhb1683

Zamora, L. P., & Wendy, B. S. (1995). *Magical Realism Theory, History, Community*. Duke University Press.